# Tanzania Dental Association

P.O. Box 65008, Dar-es-Salaam,
Tanzania,
Telephone: +255-758960550 / 0768407057
E-mail Address: [illegible]
Website: [illegible]

Office: First Floor
School of Dentistry Building
MUHAS
Dar-es-Salaam, Tanzania
Email: tanzaniadentalassociation01@gmail.com

**Kumb:** TDA/GS/13/592

01 Aprili 2023

**TAMKO LA CHAMA CHA WATAALAMU WA AFYA YA KINYWA NA MENO TANZANIA (TDA) KUHUSU TAHARUKI YA DAWA ZA MENO ZINAZOGAWIWA BURE MASHULENI**

Ndugu wananchi kuna ujumbe unaosambaa kwa njia ya mitandao ya kijamii ukiwa na picha ya kipeperushi, miswaki na dawa ya meno yenye ujazo wa gramu 15 (15gm) ukieleza kuwa jambo hili limetokea Wilaya Tunduru mkoami Ruvuma, na kuwa dawa hizi za meno zimewekewa vichocheo (hormones) zinazoweza kusababisha watoto wa kiume kuwa mashoga na wa kike kuwa wasagaji, na kuwa zinatolewa bure kwa wanafunzi wa darasa la kwanza hadi la tatu (1-3) na picha kupigwa na aliyeleta.

Chama cha Wataalamu wa Afya ya Kinywa na Meno Tanzania kimeshtushwa na kinasikitishwa na ujumbe huu ambao umezua taharuki kwa namna wananchi walivyolipokea. Kama chama cha kitaaluma chenye dhamana ya kusimamia masuala ya afya ya Kinywa na Meno Tanzania, tunaona kuna mapungufu makubwa sana kwenye ujumbe huu unaosambaa kwa lengo la kuwatahadharisha wananchi. Mapungufu hayo yanatokana na ukweli wa kutozingatia uelewa wa kisayansi, uhalisia, na malengo mahususi ya kuzuia magonjwa ya kinywa na meno ambayo hulenga makundi maalumu yaliyo katika hatari kubwa ya kuathirika. Hii inapelekea kwa sisi wataalamu wa afya ya kinywa na meno kuona kuna uwezekano mkubwa ujumbe huu umelenga kupotosha umma na unatokana na uelewa mdogo wa afya afua za kujikinga na magonjwa ya kinywa na meno, pamoja na bidhaa za kufanya usafi wa kinywa na meno. Vile vile uzushi huu unaitia doa serikali kupitia vyombo vyake mbalimbali vya kitaalam, mathalani taasisi ya uthibiti ubora wa bidhaa yaani Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI na sisi kama wanatasnia kwa kutuhumu kushirikiana na mashirika fulani fulani kuwahujumu wananchi.

Kutokana na upotoshaji huu, TDA kinapenda kuwajulisha wananchi kuwa

1. Watoto umri wa miaka 6-12 wako katika kipindi kinachojulikana kama kuwa na meno mchanganyiko ya ukubwa na ya utoto (mixed dentition). Kipindi hiki ni muhimu sana kumwezesha mtoto kupata elimu na ujuzi sahihi wa kutunza afya ya kinywa kwa meno. Hii ikiwa ni pamoja na kusafisha kinywa na meno kwa usahihi kutumia dawa ya meno yenye madini yenye kuweza kuzuia meno kuoza. Ifahamike kwamba twakimu zilizopo zinaonesha kwamba takriban watoto wote (99%) wenye umri wa miaka mitano nchini Tanzania wana dalili au athari zinazotokana na ugonjwa wa kuoza meno. Vilevile, kwa ujumla wao, takriban theluthi moja ya watoto wenye umri wa miaka 5, 12 na 15 wana ugonjwa au athari za kuoza kwa meno. Matunzo hafifu ya kinywa na meno yanaweza kupelekea maumivu makali, shida kwenye ulaji na kuongea na maambukizi kwenye eneo la kinywa ambavyo huweza

kuletelea kung'oa meno ya utoto mapema. Jambo hili lina sababisha madhara mbalimbali, yakiwemo ukuaji hafifu wa taya, mpangilio mbaya wa meno, maumivu ya kiungo cha taya, meno kulika na muonekano mbaya unaopelekea kuwa na soni na kukosa kujiamini mbele za watu. Meno ya ukubwa yakiharibika kiwango cha kushindwa kutibika kipindi hiki yakingolewa hayawezi kuota tena..

2. Shirika la Afya Duniani (WHO) linashauri matumizi ya dawa za meno zenye madini ya floridi ambayo yamethibitishwa na tafiti za kisayansi kuweza kuzuia meno kuoza. Kutokana na umuhimu wa madini ya floridi na kutokana na changamoto ya upatikanaji wake katika maeneo mbalimbali duniani, wanasayansi wameyaongeza madini ya floridi kwenye maji ya kunywa, chumvi, maziwa, vinywaji baridi, dawa maalumu za kusukutua, na dawa za meno kwa kuzingatia viwango. Hata hivyo kwa miaka mingi matumizi ya madini haya kwenye dawa za meno yameonyesha uwezo mkubwa wa kuzuia meno kuoza kutokana na upatikanaji wake na kuwafikia watu wengi kwa urahisi na kwa bei nafuu.

3. Hapa Tanzania dawa za meno zinazotumika zinathibishwa ubora na shirika la viwango (TBS) na kuandikishwa kwa mamlaka mbalimbali kabla hazijaanza kutumika. Chama cha wataalamu wa Kinywa na Meno Tanzania tunashirikiana na wazalishaji na wasambazaji wa dawa za meno ambao wamethibitishwa hapa Tanzania na waliokidhi viwango vya ubora vilivyopo. Tunaendelea kuwashauri wananchi watumie dawa za meno zenye madini ya floridi na zilizothibitishwa na shirika la ubora wa viwango Tanzania (TBS) kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa wa kuoza kwa meno.

4. Kutokana na ukweli kwamba upatikanaji wa huduma za kinywa na meno kwenye vituo vya afya hapa nchini uko chini ya asilimia 10, hivyo kuwanyima fursa wananchi wengi kupata huduma za kinywa na meno, TDA tumekuwa tukifanya kampeni ya kuhamasisha uelewa juu ya afya ya kinywa na meno kwa umma na kutoa matibabu bila malipo toka mwaka 2015 kupitia maadhimisho ya siku ya afya ya kinywa na meno duniani kila ifikapo mwezi Machi 13 mpaka 20. Wakati wa maadhimisho haya huwa tunatumia fulana, vipeperushi, mabango yenye jumbe za afya, zenye nembo ya wadhamini mbalimbali wakiwemo watengenezaji na wasambazaji wa dawa za meno zenye madini floridi pamoja na miswaki kuwafikia wananchi hasa wale wenye mahitaji maalumu, watoto, wazee pamoja na wananchi wanaojitokeza kupata elimu na huduma mbalimbali. Maadhimisho haya hufanyika kwa uwazi na hupata baraka zote za serikali kupitia Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais - TAMISEMI na kuhusisha wadau wote wanaohitajika. Toka tumeanza maadhimisho haya mwaka 2015 tumeweza kutoa matibabu, elimu na dawa za meno kwa wananchi zaidi ya 450,000. Katika kipindi chote hiki cha miaka nane wananchi tuliowafikia katika maeneo na mikoa mbalimbali ni mashahidi wa kazi kubwa inayofanywa na wanatasnia ya kutoa elimu pamoja na huduma mbalimbali za afya ya kinywa na meno, na wamekuwa wakitumia dawa hizi za meno.

**HITIMISHO**

1. Tunashauri shirika la ubora wa viwango Tanzania (TBS) na mamlaka ya chakula na dawa (TMDA) kuendelea kufanya uhakiki wa dawa za meno,

miswaki na bidhaa mbalimbali za usafi wa kinywa zilizopo hapa Tanzania na kuweka wazi majibu ya uhakiki huo kuhusiana na uzushi huu uliojitokeza.

2. Tunashauri wataalamu wa kinywa na meno, waendelee kutoa elimu ya kinywa na meno pamoja na bidhaa za usafi wa kinywa na meno kwa lengo la kuimarisha afya ya watanzania.

3. Tunaomba mamlaka ya mawasiliano Tanzania (TCRA) na vyombo vingine vya dola kufanya uchunguzi ili kubaini chanzo cha taharuki hii na kuchukua hatua stahiki na iendelee kuwaelimisha wananchi juu ya matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii.
4. Wananchi kuwa watulivu na kutokuutilia uzushi huu maanani kwani mantiki pekee inaonyesha walakini wa dawa hiyo moja iweze kutoa matokeo tofauti kwa jinsia mbili yaani kuwa kichocheo cha homoni za kike kwa watoto wa kiume na kuwa kichocheo cha homoni za kiume kwa watoto wa kike.

5. Tunaomba ujumbe huo upuuzwe na wananchi waache kuusambaza mara moja

Imeandaliwa na

TANZANIA DENTAL ASSOCIATION
P. O. Box 65008
DAR ES SALAAM

Dr Deogratias Kilasara
**RAIS CHAMA CHA WATAALAMU WA AFYA YA KINYWA NA MENO TANZANIA (TDA)**

*President: Dr.Deogratias Kilasara*
*President Elect: Dr. Gemma Berege*
*Imm. Past President: Dr.AmbegeMwakatobe*
*Hon. Secretary: Dr. Gustav Rwekaza*
*Treasurer: Dr Arnold Augustino*
*Assistant Secretary: Dr.Iddy Kheri Mnyonge*
*Editor-in-Chief: Dr.Kasusu Nyamuryekung'e*
*Member: Prof. Febronia Koku Kahabuka*
*Member: Dr. Lorna C. Carneiro*
*Member: Dr. Chermine Nasser*
*Member: Dr. David Mapunda*
*Member: Dr. Baraka Nzobo*
*Member: Dr. Leonora Asseri*
*Member: Dr.Germana Lyimo*
*Member: William Mabanga*
*Member: Dr.Muya Mgaza*
*Student Representative: TDSA President*
*Program Officer: Lilian Jonas*